# LEARNING BY EAR

## “Mizozo na utatuzi-palipo na wazee”

## Episode 9: “Vilio na nderemo”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**List of characters by scenes:**

**SCENE ONE: LAWI PAYS ELDER WALIANI A VISIT**

- **Lawi (m, 20)**
- **Waliani ( m, 75)**

**SCENE TWO: LELA AND SHANI AT THEIR FATHER’S FARM**

- **Lela ( f, 20)**
- **Shani (f, 17)**

**SCENE THREE: LAWI PAYS ELDER WALIANI A VISIT**

- **Lawi (m, 21)**
- **Waliani ( m, 75)**

**SCENE FOUR: SOMBA, KERO AND MATONGE MEET**

- **Matonge (m, 65)**
- **Somba (m, 55)**
- **Kero (f, 55)**

**Msimulizi**

**INTRO:**

Hamjambo na karibuni tena katika kipindi cha Noa bongo! Jenga maisha yako. Hiki ni kipindi cha tisa katika hadithi ya mizozo na utatuzi kwa jina, **“Palipo na wazee”.** Katika kipindi kilichopita, watorube walivamia na kutoweka na ng’ombe za wakimbebe, wakaua watu wengi na wafanyikazi wa kujitolea wa jumuia ya kimataifa. Ulimwengu mzima ulikemea tukio hilo. Kwengineko, Rais Matonge alionekana akielekea kushinda uchaguzi, hasa baada ya kuwapa silaha watorube. Lakini ni kweli atashinda? Jumuiya ya kimataifa inaweza kufanyaje ili kuzuia mauaji kama haya? Lawi ataweza kuishi na mawazo ya yale yaliotendeka? Sikiliza makini ili upate majibu katika kipindi cha leo, kwa jina, **“Vilio na nderemo”.** Tunafungua pazia kwaa Lawi akimtembelea mzee Waliani.

**SCENE ONE: LAWI PAYS ELDER WALIANI A VISIT**

1. **SFX: DOOR KNOCKING**

2. **WALIANI:** Karibu! Mlango uko wazi.

3. **SFX: DOOR PUSHED WIDE OPEN**

4. **LAWI:** Nakusalimu, mzee Waliani.

5. **WALIANI:** Nimeitika, mwanangu. Naam, kuna jambo lililotokea?

6. **LAWI:** **(takes a deep breath)** Mzigo wa kuhukumika. Nimetaka sana kutubu, lakini babangu amefurahi kwa ajili ya ng’ombe tulizozileta.

7. **WALIANI:** Twende nje, pale chini ya mti kuna kivuli kizuri.

8. **SFX: VILLAGE AMBIENCE**

9. **WALIANI:** Hakuna lisilowezekana kutatulika humu duniani . Hebu nipe hiyo bakora yangu.

10. **SFX: WALKING WITH AID OF A STICK**

11. **LAWI:** Sijui nianzie wapi, usingizi umeniruka, hamu ya kula sina, ari ya kufanya kazi pia imetoweka, akili yangu haijatulia. Ni kama ambae nataka kurukwa na akili.

**12. WALIANI:** Ni mwanamke gani huyo anayekuzuzuwa? Kwa maana ana bahati sana.

**13. LAWI:** **(Surprised)** Ah hapana, si mwanamke. Nikuhusu ule uvamizi. Mimi niliuongoza, na nikawaambia watu wangu wasisubutu kuchoma nyumba zao, lakini hawakusikia! Wasipige risasi wanawake na watoto, lakini waliingia wazimu, na wakaua chochote kilichokua hai!

**14. WALIANI:** **(sadly)** Mkasa! Huo ni mkasa mkubwa! Sasa nikusaidie na lipi? Hii ndio sababu daima tunateseka, sababu damu nyingi ya watu wasio hatia inamwagika.

**15. LAWI:** Kuna njia yeyote, mzee Waliani, njia ya kuondosha hukumu hii kichwani mwangu! Nimechoka, siwezi tena.**(breaks down in tears)**

**16. WALIANI:** Mwanamume akilia, huwa amefika mwisho. Mimi sikuhusishwa kuhusu vamizi hili. Kwanza, mungelizikataa hizo bunduki. Huyo aliyewapa bunduki hizo, alinitishia nisisubutu kuingilia mipango ya serikali.

**17. LAWI:** Alikutisha? Haikubaliki kutishia mzee wa kijiji!

**18. WALIANI:** Wakati umebadilika, mwanangu. Watu hawawathamini tena wazee, ulimwengu umewatupa. Hii ndiyo sababu ya vita hivi kila uchao. Tumesahau mila na desturi za mababu zetu! Walijuwa jinsi ya kupatanisha. Walidhamini maisha zaidi ya yote!

**19. LAWI:** Kuna njia yeyote ya maridhiano na wakimbebe? Baada ya tukio hilo? Ninahakika wanapanga kulipiza kisasi.

**20. WALIANI:** Inawezekana. Lakini munahitaji kuomba msamaha kisha kutafuta amani na wao. Kama tulivyofanya na wakoroma. Hiyo ndiyo njia pekee.

**21. LAWI:** Ki vipi? Watakubali vipi amani, baada ya watu wangu kuwaua watu wao?

**22. MSIMULIZI:** Mauaji ya Ruanda, mzozo wa Sierra Leone, mafarakano ya Afrika kusini na mikinzano mingi imetatulika kupitia amani na maridhiano. Hebu tuwarudie Lela na Shani shambani mwao, walipotembelewa na mtu ambae hawakutarajia tena kumuona.

## SCENE TWO: LELA AND SHANI AT THEIR FATHER'S FARM

**(Lela and Shani singing as they work)**

**23. LELA:** Mawingu yanafunga Shani, kutanyesha hivi karibuni.

**24. SHANI** **(relieved)** Mbegu zote zitamea tena, na hivi karibuni tutavuna. Nafurahi sana kwa kuwa tumepatanishwa na watorube.

**25. LELA:** **(shocked and in disbelief)** Shani! Hebu tazama,ni nani yule anayekuja! Ni ukweli? Ama naota?

**26. SHANI:** **(bewildered)** Mama!!!!

**27. MSIMULIZI:** Furaha, machozi, na nderemo za familia hii kukutana tena haziwezi kuelezeka. Kwa sasa lakini, nyumbani kwa Waliani, Lawi alikuwa anapata majibu yake.

**SCENE THREE: LAWI PAYS ELDER WALIANI A VISIT**

**28. SFX: VILLAGE AMBIENCE**

**29. WALIANI:** Eleza ukweli! Ukweli utakuweka huru. Sio rahisi kusema ukweli, sio rahisi kusikia ukweli. Lakini baadaye huleta uponyaji na maridhiano.

**30. LAWI:** **(shocked)** Una maana niende hadi makao ya Kimbebe, niwatake wakusanyike alafu niwaambie: “Jamanini, samahani. Lakini ni sisi ndio tulihusika na vifo vya mamia ya watu wenu?” Watanichuna ngozi kisha wanizike mzimamzima!

**31. WALIANI:** Simaanishi hivyo. Kawaida jambo kama hilo likitokea, kwanza watu waaminifu, wenye hekima na busara huchaguliwa kuongoza mikutano ya amani na maridhiano.

**32. LAWI:** Nani? Nani hapa anaweza kuaminiwa? Yupi ambae hatapendelea upande mmoja, ambaye ni mkweli na mwenye busara? Tunaweza kuamini wazee kama nyinyi tu, lakini mumebakia wachache sana.

**33. WALIANI:** Sio lazima wawe wazee, wanaweza kuwa viongozi wa kidini , wanasiasa au hata mawakili.

**34. LAWI:** Tutakuchaguwa wewe! Baadaye huwa kunatokea nini?

**35. WALIANI:** Alafu waasi na wale walidhulumiwa wote wanaketi chini kuzungumza ukweli kuhusu mauaji hayo. Ni suala ambalo hisia za kila aina zitatolewa, lakini uzuri ni kuwa mkutano utaisha ikiwa pande zote mbili zina amani.

**36. LAWI:** Alafu adhabu? Adhabu ya wale waliotenda uhaini?

**37. WALIANI:** Wakati wetu kulikuwepo na adhabu aina nyingi. Kama kwenye kisa kama hiki tungelitumia “kinywaji kikali cha miti shamba” .

**38. LAWI:** Kinywaji kikali? Sijasikia adhabu kama hiyo.

**39. WALIANI:** Ni mambo marefu, kwanza muhusika anakubali kuwa alifanya ukatili huo, anatubu, anaomba msamaha na kulipa fidia. Kisha, wanaporidhiana, wote wahini na wahiniwa wanakunywa pamoja maji ya mzizi mkali. Hii ni ishara ya uchungu walioupitia katika maridhiano hayo.

**40. LAWI:** Na hiyo dawa kali kweli ingelileta suluhu?

**41. WALIANI:** Siyo dawa kali pekee. Watu wenyewe watatuwa mzozo huo. Enzi zetu, tulisististiza sana utu. Waafrika wote waliamini kutoka kwenye kizazi kimoja. Maneno kama, “ujamaa” kwa kiswahili. “Kparakpor” ki Yoruba, “ubuntu” ki Zulu, “umma” ki Arabu, pamoja na lugha nyengine na utamaduni: humaanisha jumuiko la watu wamoja.

**42. LAWI:** Nilitaka tu kuregesha ng’ombe za babangu. Sikunuia kuua yeyote. Hasa watoto na wanawake.

**43. WALIANI:** Fanya mambo yawe sawa basi, na yatatatulika. Tuma mjumbe akawaalike watorube kwa sherehe ya amani na maridhiano, mimi nitauongoza.

**44. LAWI:** Nakushukuru mzee Waliani. Umenisaidia sana.

**45. NARRATOR:** Lawi alimuaga mzee Waliani nyumbani kwake, akaenda moja kwa moja hadi kwa babake Masambo nakumuarifu yote. Masambo aliungana na mwanae na ghafla kijiji kizima kikahusishwa. Mjumbe alitumwa na ujumbe wa kukutana ndani ya msitu kwa mazungumzo hayo ya amani na maridhiano. Kwengineko, mambo yalianza kupamba moto kwa kina Kero, Somba na Rais Matonge, ambao walikuwa wana mashtaka ya kujibu katika mahakama ya kimataifa ya hague, kwa kufadhili, kuyaunga mkono na kuchochea uhaini dhidi ya binaadamu.

**SCENE FOUR: SOMBA, KERO AND MATONGE MEET**

**46. KERO:** Naam, muheshimiwa Rais. Umetuita kwa mkutano wa dharura.

**47. SFX: LETTER BEING OPENED (studio)**

**48. MATONGE:** **(furious)** Kero, Somba, mumesoma haya? Huu ni upuuzi gani ninaosikia? Muliniambia nisihofu! Sasa! Mbona sote watatu tunatakiwa kujibu mashtaka katika mahakama ya kimataifa ya uhalifu ICC, The Hague?

**49. SOMBA:** ICC? Ni kina nani hao.? Mbona watufungulie mashtaka? Kwanza, iko wapi hiyo The Hague? Hata mimi nilipata barua hiyo.

**50. KERO:** **The** Hague iko nchini Uholanzi ambako ICC, au mahakama ya kimataifa ndiko iliko. Ilianzishwa mwaka wa 1998 kwa nia ya kuwapa haki walioathiriwa na uhalifu wa kivita , mauaji ya watu bila sababu na uhaini wowote unaofanyiwa binadamu. Wanataka tujibu maswali kuhusu uvamizi wa Kimbebe, wapuuze muheshimiwa Rais.

**51. MATONGE:** Nyinyi munaishi ulimwengu gani lakini? Hamujui kuwa akaunti zangu zote za benki zilizo ng’ambo wamezizuia ? Pia wametuzuia hata kusafiri! Sisi ni wafungwa wa humu kwetu nchini!

**52. KERO:** Muheshimiwa Rais..

**53. MATONGE:** **(angry)** Usinipake mafuta kwa mgongo wa chupa Kero! Nataka kujuwa ukweli, kulitokea nini katika uvamizi huo? Naweza kuitwa kiongozi wa ki-imla lakini mimi si muuaji wa watoto!

**54. SOMBA:** Uliamuru bunduki zipatiwe raia . Ulitarajia nini? **(sarcastic)** kwamba watazitumia kama bakora?

**55. KERO:** Tulifanya haya ili ubakie mamlakani!

**56. MATONGE:** Nyote nimewafuta kazi! Tangu sasa, hamufanyi tena kazi katika serikali yangu!

**57. KERO:** **(threatening)** Umechelewa kutufuta kazi, labda haufahamu ICC inahusu nini. Hii sio korti kama hizi hapa, ambako tunaweza kuhonga majaji na kuachwa huru.

**58. SOMBA:** Kero anasema ukweli, tumebaki na chaguo moja tu.

**59. MATONGE:** Ati? Chaguo gani hilo?

**60. KERO:** Kuenda mafichoni, tukajifiche na tuombe wasitupate.

**61. MATONGE:** Siendi kokote. Hii ni nchi yangu, nilizaliwa hapa! Nitakufa hapa! Kwisha!

**62. KERO:** Kazi kwako, Matonge, lakini mambo sio mazuri vile. Watu wengi hawaridhishwi na serikali yako, na uvamizi wa Kimbebe umewakasirisha wapiga kura.

**63. MATONGE:** Unasema nini? Si ni jana tu, kura za maoni zilionyesha ni mimi watanichagua.

**64. SOMBA:** Hiyo ni kabla ya kusikia hizo habari.

**65. KERO:** Nimeshapanga kila kitu. Lakini ni lazima tutoroke humu nchini haraka iwezekanavyo. Watu tayari wanakutana katika uwanja wa uhuru kupanga maandamano. Heri tuondoke kabla mambo hayajaharibika.

**OUTRO:**

Mibabe mitatu ya kisiasa, iligeuka na kuwa wakimbizi, wakiikimbia sheria. Lakini watafika umbali gani? Katikati ya mpaka wa bonde la Kijani na mpaka wa maeneo ya Kimbebe, mkutano wa kweli na maridhiano umeanza. Utazaa matunda? Majibu yote yako katika kipindi cha kumi cha hadithi ya mikinzano na utatuzi kwa jina, **“Palipo na wazee”.**Ukitaka kusikiliza kipindi hiki au vilivyotangulia, tembelea tovuti yetu www.dw-world.de/lbe. Mpaka wakati huo. Kwaherini.